Ecolebooks.com

MWONGOZO WA KARATASI YA PILI, KASSU. (KISWAHILI PAPER 2 MARKING SCHEME)

1. Ufahamu

a. Thibitisha kwamba Covid-19 umezia utangamano wa kimataifa. (Alama 1)

Shughuli za kimataifa zilitatizika kwa njia zisizomithilika

b. Eleza kinaya inayojitokeza kwa Covid-19 na wahudumu wa afya. (Alama 1)

Wahudumu wa afya walikosa nafasi ya matibabu au nafasi ya kulazwa katika hospitali wanazohudumu wenyewe.

c. Covid -19 umesababisha madhara mengi ya kiuchumi. Thibitisha ukweli wa kauli hii kwa hoja tatu. (Alama 3)

1. Watu wengi kupoteza kazi zao.

2. Watu wengine kutuma kwa likizo bila malipo.

3. Wengine kukatwa mishahara kwa asilimia kubwa.

4. Biashara nyingi kufungwa nyingi zikipata hasara chungu nzima.

5. Benki kuathirika kwa wateja kushindwa kulipa mikopo.

d. Taja dalili zozote mbili za maambukizi ya virusi vya korona. (Alama 1)

1. Kukohoa

2. Kushindwa kupumua au ugumu wa kupumua

3. Joto jingi au baridi kali mwilini

4. Maumivu ya misuli au mwili,

5. Kutapika au kuendesha, kupoteza hisia za kuonja na kunusa

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON **ECOLEBOOKS.COM**

Ecolebooks.com

e. Eleza matendo matatu kulingana na kifungu hiki ambayo yanamweka mtu kwenye hatari ya maambukizi ya ugonjwa huu (Alama 3)

1. Kutovaa barakoa kila wakati unapoenda kwenye watu.

2. Kutokuosha mikono yako kwa maji yanayotiririka na sabuni au kuitakasa.

3. Kwenda kwenye mikusanyiko ya watu.

4. Kutozingatie umbali wa mita moja unapokumbana na watu.

f. Taja mikakati miwili iliyowekwa na serikali ya Kenya kukabiliana na virusi hivi. (Alama 2)

1. Serikali ilitangaza kufungwa kwa shule.

2. Kafyu ya saa moja usiku hadi saa kumi na moja asubuhi iliwekwa hapo awali

3. Kufungwa kwa uchukuzi wa kimataifa ulitangazwa

4. Kudhibitiwa kwa uchukuzi nchini kwa kupunguzwa kwa idadi ya watu kwenye uchukuzi wa uma.

5. Mikusanyiko ya watu ulipigwa marufuku

6. Kanisa kufungwa japo kwa muda.

7. Idadi ya watu katika arusi na mazishi kupunguzwa mno.

8. Maeneo ya burudani pia yalifungwa kwa muda

g. Serikali ya Kenya ililegeza mikakati yake vipi? (Alama 1)

1. Saa za Kafyu zilipunguzwa

2. Uchukuzi wa kitaifa na kimataifa ulifunguliwa upya.

3. Shule pia zilianza kufunguliwa japo kwa watahiniwa.

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON **ECOLEBOOKS.COM**

Ecolebooks.com

4. Kufunguliwa kwa maeneo ya burudani

5. Maeneo ya kuabudu yalifunguliwa japo kwa masharti ya kiafya.

h. Eleza maana ya maneno yafutayo jinsi yalivyotumika kifunguni (Alama 2)

i) Kafyu

Amri ya kutotoka nje nyakati fulani haswa usiku hadi asubuhi kama ile ya usiku hadi asubuhi

ii) Mchakato

Hatua za kufuata wakati kufanya jambo kama hatua za kutafuta za kutafuta chanjo.

2. Ufupisho

a) Faida za mitandao ya kijamii

1. Mitandao ya kijamii imerahisisha mawasiliano.

2. Biashara kitaifa na kimataifa imemarishwa na mitandao ya kijamii.

3. Ni muhimu pia kutambua kuwa, mitandandao ya kijamii hukuza umoja na ushirikiano wa watu na vile uzalendo.

4. Mitandao ya kijamii imezidi kukuza na kuendeleza demokrasia.

5. Walimu wanaweza kuwafundisha wanafunzi moja kwa moja kwa mitandao ya Kijamii (Huimarisha elimu.

6. Ikumbukwe mitandao ya Kijamii ni nyenzo muhimu ya kueneza habari.

7. Habari za kimataifa pia hueneza zaidi mitandaoni.

8. Wasanii wengi wamenufaika kwa mitandao hii kama nyenzo ya kipato cha kila siku,hivyo basi imeunda nafasi za ajira.

9. Mitandao ya kijamii pia imetoa nafasi pana ya burudani kwani watu wengi hupata kufurahishwa na kuchekeshwa na wasanii mitandaoni humo.

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON **ECOLEBOOKS.COM**

Ecolebooks.com

*Hoja zozote 8 (1*8)*

b) Fupisha aya tatu za mwisho

1. Mitandao ya Kijamii ina hasara kando na kuwa na faida nyingi

2. Vijana, hata wenye umri wa miaka chini ya kumi na nane wamejiingiza kwa mapenzi.

3. Kando na hayo, mitandao hii imesababisha utovu wa maadili.

4. Utapeli ni mwingi mitandaoni.

6. Watu wanaweza pia kueneza habari za uwongo mitandaoni na kusababisha mizozo.

7. Ni muhimu pia kutambua uzembe na uvivu kama hasara inayosababishwa na mitandao ya Kijamii.

8. Vijana wengi huwa tu kwa simu na vipakatalishi siku kutwa na hata usiku kucha bila kufanya kazi ama hata kusoma.

9. Uchochezi wa kisiasa huenezwa humo pia. Watu ambao wangeishi kwa amani huanza vita kutokana na uchochezi mitandaoni.

10. Mitandao ya Kijamii hukumbwa na changamoto nyingi.

11. Moja ni ukosefu wa nguvu za umeme. Si watu wote

13. Upungufu wa fedha kutokana na ufukara husababishwa watu kukosa kununua simu au vipakatilisha au hata kukosa pesa za mjazo.

14. Zaidi ya hayo ni kutoenea vya kutosha kwa mitandao mbali mbali na hivyo kutowafikia watu wote.

15. Sera za kudhibiti matumizi matumizi ya mitandao ya Kijamii zingali ni finyu na changamamoto za kisheria.

16. Ni muhimu kutumia mitandao hii kwa manufaa yetu wala si kutudhuru.

3. Matumizi ya lugha

a)(1) Tofautisha kati ya ala tuli na ala sogezi kwa kutolea mifano moja moja (Al. 2)

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

Ala tuli ni ala zisizosogea wakati wa kutamka kwa mfano meno, ufizi, kakaagumu, kaakaalaini, koromeo ilhali ala sogezi ni ala za kutamkia zinazosogea wakati wa matamshi kwa mfano midomo na ulimi.

(1×2=2)

(2) Tambua sauti zenye sifa zifuatazo : (Al. 2)

i) irabu ya chini wastani - **/a/**

ii) Sauti ambayo ni irabu na konsonanti vile vile **- /w/,/y/**

iii) Kizuiwa-Kikwamizwa **-/ch/**

iv) Sauti tandaze ya mbele ,kati ya ulimi **-/e/**

(1×4=2)

b). Eleza tofauti iliyopo kati ya silabi wazi na silabi funge (Al.1)

Silabi wazi ni silabi inayoisha kwa irabu ilhali silabi funge huisha kwa konsonanti.

(1×1=1)

c) Tunga sentensi yenye kiunganishi cha masharti (Al. 1)

Ukisoma kwa bidii utafaulu.

(1×1=1)

d)Geuza kirejeshi katika sentensi ifuatayo ili kuleta dhana ya hali ya mazoea (Al.1)

Wanafunzi ambao wanasoma kwa bidii watatuzwa

Wanafunzi wasomao kwa bidii watatuzwa

(1×1=1)

e) Eleza maana mbili zinazojitokeza katika sentensi ifuatayo : (Al. 1)

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON **ECOLEBOOKS.COM**

Ecolebooks.com

Pika chakula kingine

1. Kuongeza /ziada ya

2. Badala ya /kibadala cha /tofauti na

(½×2=1)

g) Kwa kuzingatia uamilifu, taja kwa kutolea mifano aina zozote nne za sentensi za Kiswahili (Al. 2)

1. Sentensi ya swali

2. Sentensi ya hisia /mshangao

3. Sentensi ya ombi /rai

4. Sentensi ya amri

5. Sentensi ya taarifa

(½×4=2)

h) Tilia shada katika maneno yaliyopigiwa mstari katika sentensi zifuatazo : (Al. 1)

i) Alifanya kazi yake **ba'rabara**

ii) Mwimbaji alijinunulia **a'la** za muziki.

(½×2=1)

i) Yakinisha kwa wastani (Al. 2)

Janajike lile halijanunua majitabu mazuri

Mwanamke yule amenunua vitabu vizuri

(2×2=2)

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON **ECOLEBOOKS.COM**

Ecolebooks.com

j) Tunga sentensi ya neno moja yenye viambajengo vifuatavyo : (Al. 2)

Nafsi ya pili wingi,mzizi, kauli ya kutendesha, kauli ya kutenda , 'o'rejeshi tamati

Msomeshao

Hakiki majibu ya mwanafunzi

(1×1=1)

k) Fafanua miundo mitatu ya ngeli ya A-WA kwa kutolea mifano mahususi (Al. 3)

M -wa :Mtu -watu

M -Mi :Mtume -Mitume

Ki -Vi :Kifaru -Vifaru

Ch -Vy :Chura -Vyura

Kapa -Ma :Daktari -Madaktari

(1×3=3)

l) Ainisha viambishi awali na tamati ; (Al. 2)

Waliwao - **Wa - awali**

-iwao -tamati (½×2=1)

Msioabudu - **msio -awali**

u -kiambishi tamati (½×2=1)

m) Tambua aina za shamirisho; (Al. 3)

Mama mzee alijengewa nyumba ya kifahari na mjukuwe kwa mawe

Mama mzee -kitondo

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON **ECOLEBOOKS.COM**

Ecolebooks.com

nyumba ya kifahari -kipozi

mawe -ala

(1×3=3)

n) Ainisha virai katika sentensi ifuatayo (Al. 3)

Mwalimu huyo alikuwa akiandika kitabu kikubwa mno jana jioni.

1. RN-Mwalimu huyo

2. RT-alikuwa akiandika

3. RN -kitabu kikubwa

4. RV- Kikubwa mno

5. RE -mno jana jioni

6. RT -alikuwa akiandika kitabu kikubwa mno jana jioni

7. RN - kitabu kikubwa mno j

Atambua aina zozote 6 (½×6=3)

o) Tunga sentensi moja kuonyesha maana mbili za neno "kaa" (Al. 2)

1. Mnyama wa majini

2. Kitendo cha kuketi

3. Pande la kuni lililochomwa

4. Kushinda mahali fulani

(1×2=2)

p) Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya jedwali (Al. 4)

Wakulima wakipata pesa wataanza kazi

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

		S		
KN			KT	
N	Ś		T	N
Wakulima	wakipata pesa		wataanza	kazi.

(1×4=4)

q) Tunga sentensi moja kuonyesha matumizi mawili ya kiambishi "-ji" (Al. 2)

1. Uundaji wa nomino kutoka kitenzi - uimbaji, mwimbaji

2. Mtendwa - amejipikia

3. Ukubwa - jitoto, jitu

Atungie sentensi MOJA

(1×2=2)

r) Eleza matumizi ya kibainishi kwa kutolea mifano katika sentensi (Al. 2)

Ritifaa

1. Ufupishaji wa maneno/tarakimu - 'ndo badala ya ndio , '63-1963

2. Kuonyesha sauti ya ving'ong'o - ng'ombe

3. Kuonyesha silabi iliyotiliwa mkazo - ba'rabara

(1×2=2)

s) Andika kwa usemi halisi (Al. 3)

Mwalimu alishangaa na kutaka kujua kwa nini wanafunzi hawakuwa wameelewa mada hiyo siku hiyo (Al. 3)

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON **ECOLEBOOKS.COM**

Ecolebooks.com

"Ala! Kwa nini hamjaelewa mada hii leo? " Mwalimu akauliza.

Hakiki matumizi ya vihisishi vinginevyo

(1×3=3)

3. ISIMUJAMII

a. Eleza maana za istilahi zifuatazo : (Alama 2)

i) sajili **- ni muktadha mbali mbali ya matumizi ya lugha**

ii) lahaja **- ni vilugha vidogo vidogo vinavyotokana na lugha moja kuu.**

(1×1=2)

b. Taja nadharia tatu za chimbuko la Kiswahili (Alama 3)

1. Kiswahili ni lugha ya Kiafrika yenye asili ya Kibantu

2. Kiswahili ni lahaja ya Kiarabu

3. Kiswahili ni lugha ya mseto

c.(i) Eleza maana ya dhana usanifishaji (Alama 1)

Ni uteuzi na uimarishaji wa lahaja moja ya lugha miongoni mwa lahaja nyingine ili kutumika katika shughuli rasmi.

(1×1=1)

(ii) Fafanua sababu mbili za usanifishaji wa Kiswahili . (Alama 2)

1. Kuwepo kwa lahaja nyingi za Kiswahili

2. Kulikuwa na hati tofauti zilizotumiwa kuandika Kiswahili

3. Shughuli mbali mbali za kidini

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON **ECOLEBOOKS.COM**

Ecolebooks.com

4. Haja ya kusawazisha maandishi ya kitaaluma

5. Haja ya kuwa na lugha moja ya mawasiliano na elimu

(1×1=2)

d. Eleza dhima mbili za lugha lugha rasmi. (Alama 2)

1. Kuendesha shughuli zote katika ofisi za serikali

2. Kufundisha shuleni.

(1×1=2)

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON **ECOLEBOOKS.COM**